



**Taarifa kwa Vyombo vya habari
Imezuiliwa hadi tarehe 1 Aprili 2014**

Fedha zinamiminika, maji kiduchu Upatikanaji wa maji safi hauboreki licha ya uwekezaji mkubwa

Tarehe 1 Aprili 2014, Dar es Salaam: Bajeti kwa ajili ya kuboresha huduma ya sekta ya maji imeongezeka karibu mara tano kati ya mwaka 1999/2000 na mwaka 2011/2012, lakini hakujawa na ongezeko la tarakimu wala ubora wa upatikanaji wa huduma ya maji safi katika kipindi hicho. Kinyume chake, kati ya mwaka 1990 na 2011, upatikanaji wa huduma ya maji ulishuka kutoka 55% hadi 53%. Vile vile, kati ya mwaka 1995 na 2005, Tanzania ilipokea misaada kwenye sekta ya maji inayolingana na dola za Kimarekani 57 kwa kila anayenufaika bado upatikanaji wa huduma ya maji ulishuka kwa 1%. Ikilinganishwa na nchi nyingine, Uganda ilipokea dola 16 kwa kila anayenufaika katika kipindi hicho hicho na walifanikiwa kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa 25%, wakati Kenya ilipokea dola 17 kwa kila anayenufaika na walipata ongezeko la upatikanaji wa maji kwa 20%.

Matokeo haya yametolewa na Twaweza kwenye muhtasari wa utafiti wenye jina la “*Fedha zinamiminika, Maji kiduchu. Changamoto za upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania*”. Muhtasari umetokana na takwimu kutoka *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kaya wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu ya mkononi Tanzania bara.

Kukosekana kwa maboresho katika upatikanaji wa maji safi kwa zaidi ya miaka 20 pia ni kinyume na mwenendo wa maeneo mengine ya Afrika, ambako upatikanaji umeongezeka - kutoka 49% mwaka 1990 hadi 63% mwaka 2011. Kutokana na kushuka kwa upatikanaji wa maji safi licha ya uwekezaji mkubwa, kufanikisha malengo makubwa ya *Matokeo Makubwa Sasa (BRN)* ya kufikia 75% ya Watanzania wanaopata maji safi na salama itahitaji mabadiliko makubwa kiutendaji. Kuongeza fedha kwa ajili ya sekta ya maji bila kufanya mapitio ya kina kujua sababu za kushindwa kutoa huduma siku za nyuma, kunaweza kusababisha makosa ya zamani kujirudia.

Karibu Mtanzania mmoja kati ya watatu (30%) anasema kuwa maji ni moja kati ya matatizo matatu makubwa yanayoikabili nchi yetu. Pengine haishangazi kutokana na ukweli kuwa hakuna maboresho ya upatikanaji wa maji kwa kipindi kirefu. Maji yamewekwa nafasi ya juu pamoja na afya kama changamoto ya msingi kwa Watanzania. Suala pekee ambalo wananchi walidai ni changamoto zaidi ni uchumi (43%).

Changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama imeendelea kuwepo kwa watu wengi. Karibu Watanzania wote (89%) huchota maji kutoka vyanzo vya umma, hii ina maana kuwa ni mtu mmoja tu kati ya kumi (11%) ndiye mwenye bomba la maji nyumbani au maji yanaletwa nyumbani. Lengo rasmi la Serikali ni kuona watu wanatumia si zaidi dakika 30 tu (safari ya kwenda na kurudi) kuchota maji, lakini wastani wa muda halisi wanaotumia ni karibu saa moja (dakika 57).

Sauti za Wananchi pia iliuliza ni nani mwenye jukumu la kuchota maji kwenye kaya: katika kaya tatu kati ya nne, mwenye jukumu hilo ni mwanamke mkuu wa kaya ambaye ni lazima ahakikishe kuwa kaya ina maji kwa ajili ya mahitaji ya kila siku.

Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisema *“Ikilinganishwa na uwekezaji mkubwa katika sekta ya maji kupungua kwa upatikanaji wa maji safi na salama kunatisha. Kama tunahitaji kufanikisha malengo ya Matokeo Makubwa Sasa, tunahitaji tathmini ya haraka kujua makosa gani yalifanyika, kipi kilikwenda mlama na fedha zilifanyia nini.*

---- Mwisho ----

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Risha Chande

Meneja Mawasiliano, Twaweza

Baruapepe: rchande@twaweza.org | **Simu:** (+255) (0) 656 657559

Maelezo kwa Wahariri

- Muhtasari huu na takwimu zilizomo zinapatikana hapa www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayomlenga raia na inayokusudia kuleta mabadiliko makubwa Afrika Mashariki. Twaweza inaamaini kuwa mabadiliko ya kudumu hayana budi kuanzia chini kwenda juu. Tumedhamiria kujenga mazingira na kupanua fursa ambazo zitatoa mwanya kwa mamilioni ya watu kuhabarishwa na kuwawezesha kuweza kuleta maendeleo katika jamii zao moja kwa moja na kuifanya Serikali iwajibike.
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:
Tovuti: www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza_NiSisi